



TANJEMA

UJUMBE

Kitabu hiki cha hadithi ni chapisho la Filamu fupi ya TANJEMA iliyoandaliwa kutokana na utafiti wa awali wa maadili na uadilifu miongoni mwa watoto uliofanywa katika shule 10 za wilaya za Temeke na Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Maudhui ya filamu hii yaliandaliwa na wabunifu wa mashirika ya TEDI, Tai Tanzania kwa ushirikiano baina ya TAKUKURU na timu ya wahitimu wanne kutoka Mandela Washington Fellowship for Young African Leadership Initiative maarufu kama YALI, inayoundwa na ndugu Frederick Fussi (2016), Gloria Anderson (2021), Ian Tarimo (2019) na Sarah Chodota (2021).

Maudhui ya chapisho hili na filamu ya TANJEMA yamekusudia kuhamasisha tabia njema miongoni mwa watoto. Falamu inawapa watoto nyenzo za kufikiri kwa kina ili kukuza maadili, uadilifu na hatimaye kujiepusha na vitendo vya rushwa wangali wakiwa wadogo.

Walimu na wanafunzi pamoja na watoto wote kwa ujumla wanahamasishwa kutumia chapisho hili kuibua mjadala na kuchochea fikra zinachangia katika kuimarisha nidhamu, maadili na uadilifu maeneo ya nyumbani, shuleni na kila sehemu ya maisha ya kila siku.

TANJEMA imedhaminiwa na U.S Department of State chini ya Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam kama sehemu ya utekelezaji wa mpango wa Wahitimu katika Ubunifu ya mwaka 2022 yaani (the 2022 Alumni Engagement Innovation Fund)

WASHIRIKA:



WATAJARISHAJI:



TAI PLUS
dar es salaam, tanzania
business@taiplus.co.tz

MWANDISHI: PADILI A. JAMES


MCHORAJI: ARAFAT BRAVOO PHOENIX Sr.

MSANIFU: VICTOR J. LYAMUYA


KATIKA KIJIKI CHA ADILI, TEKNOLOJIA, MICHEZO NA MAADILI NI SEHEMU YA TAMADUNI. HIVYO, WATOTO NA WATU WAZIMA WANALAZIMIKA KUJIFUNZA NA KUWA WABUNIFU.



MTAA WA MWENDAZAKE ULIKUWA NA WATOTO WENYE VIPAJI VYA UBUNIFU WA VIFAA VYA KUCHEZEA KAMA VILE MAGARI, HASA HASA WATOTO WAWILI, TANJEMA NA LINDI.



TANJEMA (10) NI MTOTO, MBUNIFU, MWENYE UPENDO NA MICHEZO YA MAGARI. FAMILIA YAKE, IMEMFUNDISHA KUWA MTOTO WA KUFUATA SHERIA, TARATIBU NA MAADILI MEMA.



LINDI, TANJEMA NA SAI WALIKUWA NA UWANJA WAO MAALUM WA KUCHEZEA, WALIOUTENGENEZA WENYEWE NA KUJIFUNZA MAMBO MBALIMBALI YA UBUNIFU.





SIKU HIYO, LINDI NA TANJEMA, WALIKUWA NA MICHUANO YA MASHINDANO YA MAGARI. TANJEMA ALIPANIA KUSHINDA NA LINDI PIA ALIAPA KUTUMIA KILA NJIA KUSHINDA.




JINAMIZI LA HONGO, LILIKUWA LINAWANYEMELEA, KUHARIBU ARI NA UMOJA WAO KATIKA UBUNIFU NA MICHEZO.



JINAMIZI HONGO AKITUMIA NGUVU ZAKE KUHARIBU HAKI NA MAADILI
KATIKA MCHEZO HUU WA UBUNIFU NA HAKI.







**SAI NA LINDI WAKIJIANDAA KUANZA MASHINDANO YAO YA FAINALI
AMBAYO MSHINDI ATACHUKUA GARI LA MWENZAKE.**




**NA KATIKA ULIMWENGU WA MIDOLI(MADEREVA), NAO PIA WAKIWA
TAYARI KWA MASHINDANO.**





TWENDEE...

NA MADEREVA WOTE WAWILI WANABONYEZA VITUFE VYAO NA KUANZA MASHINDANO KWA SPIDI YA KASI SANA.



CLICK

CLICK




VRUUUUUUUM

VRUUUUUUUM



MBONA GIA HAINGII...JAMANI!!

KATA KONAAAA...
KATA KONA..KIMBIAAA
SPIDIII...




TUNAONA TANJEMA AKIONGOZA MBIO HIZI ZA MAGARI, LAKINI LINDI KWA KUKUSUDIA KABISA ANAGONGA UBAVU WA GARI LA TANJEMA.




TAA YA KUVUNJA SHERIA IKIWAKA, LAKINI SAI KWA MAKUSIDI ASEMI CHOCHOTE.

SAAAI.
HUONI LINDI
ALIVYONIGONGA.



TWENDE
TANJEMA BHANA,
ENDESHA.


NA LINDI ANAMUACHA TANJEMA KWA UMBALI MREFU NA KUONGOZA MASHINDANO HAYA YA MBIO ZA MAGARI.




LAKINI TANJEMA HAKUKATA TAMAA NA ANAMKARIBIA LINDI KWA MARA NYINGINE TENA, AMAKWELI MASHINDANO HAYA YAMEPAMBA MOTO.





NA SASA MAGARI YOTE MAWILI YANAONEKANA YAKIINGIA NDANI YA HANDAKI..



TANJEMA ANAMPITA LINDI KWA KASI SANA, LAKINI LINDI HAKUBALI NA KUMSOGELEA KWA UKARIBU.



LINDI ANA WASIWASI WA KUSHINDWA SHINDANO HILI NA ANACHUKUA MAAMUZI YA KUVUNJA SHERIA KWA MARA NYINGINE TENA NA KULIGONGA GARI LA TANJEMA.




TAA YA KUVUNJA SHERIA INAWAKA TENA, NA SAI BADO HAFANYI MAAMUZI YEYOTE.



TANJEMA ANACHOSHWA NA UVUNJAJI WA SHERIA UNAOENDELEA, NA KUPIGA CHINI RIMOTI YA LINDI.



AAAH TANJEMA.
UMEHARIBU RIMOTI
NA WEWE.



LIONEEE.
WIVU UMEKUJAA TANJEMA.
UMENIONA NINASHINDA UKAHARIBU
MCHEZO. SHERIA SHERIA KILA
SIKU, HUIKUJUI KUENDESHA GARI.




SAI,
LINDI KANIGONGA
MARA MBILI NA
UMEMWACHA TU BILA
KUMSIMAMISHA NA
KUMKATA POINT.
SITAKI KUCHEZA
TENA.



KWANI LAZIMA KUFUATA SHERIA KILA SIKU? UTAKUFA? UTAKONDA?


NACHUKIA KUCHEZA NA NYIE MSIOFUATA SHERIA.



MKANDAMIZENI TU TANJEMA.

LINDI UNATAKA USHINDE NA SAI UNATAKA GARI ZURI. KWANI KUNA UBAYA.






WE TANJEMA
SI UPOTEZEE
TU.



WEEEEEE.
ACHIA GARI
LANGU.



LEO, UTAONA.
SIACHII, UMEZOEA
KUDHULUMU
HAKI ZA WATU.


MZEE MAADILI HAKUFURAISHWA NA UVUNJAJI WA SHERIA NA HAKI ULIOKUA UNAENDELEA, NA ANAAMUA KUINGILIA KATI.



ACHENI
KUGOMBANA
HARAKA.








UPENDELEO,
UBINAFSI UNAHARIBU
LISTAWI WA URAFIKI
WENU.

KUMBE BADO KUNA
WANADAMU WANAJOJUA
THAMANI YA MAADILI NA
KUTENDA HAKI. DAAH,
RUSHWA NI MBAYA
SI MCHEZO. ONA,
MZEE KANIUA
TAYARI.



TANJEMA, LINDI NA SAI - WALIKUBALI KUFUNDISHWA NA KIJENGA
UHUSIANO WAO KATIKA MICHEZO VIZURI NA KWA AMANI.



ṬIMIZA WAḶIBU ṬENDA HAKI ṬII SHERIA



MANDELA
WASHINGTON
FELLOWSHIP
FOR YOUNG AFRICAN LEADERS

